



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
IDARA YA UHAMIAJI



Tarehe: 13 Aprili, 2026

TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU KUITWA KWENYE MAFUNZO

1. Kamishna Jenerali wa Uhamiaji anawatangazia vijana walioomba Ajira na kuitwa kwenye usaili kupitia Mfumo wa e-Ajira wa Uhamiaji kwamba wale waliochaguliwa wametumiwa ujumbe kupitia barua pepe na simu zao kuwa wanatakiwa kujiunga kwa ajili ya Mafunzo ya Awali ya Askari wa Uhamiaji ambayo yatatolewa katika Chuo cha Uhamiaji cha Raphael Kubaga kilichopo Wilaya ya Mkinga Mkoa wa Tanga. Ujumbe huo umeanisha siku, tarehe na muda wa kuripoti chuoni.
2. Wakati wa kuripoti Chuoni mhusika atalazimika kuonesha ujumbe wa simu au barua pepe ya wito wa kujiunga na mafunzo husika. Aidha, vijana hao wanatakiwa kuwa na Uthibitisho wa kuwa yeye ndiye mhusika halisi kama vile Kitambulisho cha Taifa, Kitambulisho cha Mkaazi au Pasipoti ya kusafiria. Sambamba na hilo, mhusika anatakiwa kuwa na nyaraka halisi za Cheti cha kuzaliwa, vyeti vya taaluma, Kitambulisho cha taifa pamoja na nakala zake.
3. **Mahitaji na vifaa Vingine vinavyohitajika ni kama ifuatavyo:-**

NA	MAHITAJI
1.	Bima ya Afya yenye uhai
2.	Fedha ya Bima ya Afya tsh 50,400/= kwa wasio na bima ya afya
3.	Shuka na foronya rangi ya blue Nne(4)
4.	Mto
5.	Chandarua cha duara (light blue)
6.	Sanduku la bati kubwa (Tranka)
7.	Ndoo kubwa na ndogo
8.	Truck suit rangi nyeusi na Blue pair moja kila rangi
9.	Raba pair mbili kwa aiili ya michezo(rangi yeyote)

Ofisi ya Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Eneo la Uzunguni, 4 Barabara ya Mwangosi, S. L. P. 1181, Dodoma.
Simu: +255 262323542/+255 262323543, Nukushi: +255 262323532
Barua pepe: info@immigration.go.tz Tovuti: www.immigration.go.tz

10.	Nguo chache nadhifu
11.	Rain Boot pair moja kijani/ Nyeusi
12.	Counter Book (4) - Four Quire
13.	Vifaa vya usafi (Jembe, Sururu, Kwanja, Panga na Mfagio wa chelewa).
14.	Fedha ya kujikimu

4. Aidha, vifaa vifuatavyo pia vinapatikana katika duka la Chuo; shuka na foronya, chandarua, t-shirt, tranka, ndoo kubwa na ndogo, counter book four quire, rain boot kijani/nyeusi, vifaa vya usafi pamoja na mahitaji mengine.

5. Kwa changamoto, tafadhali wasiliana nasi kupitia: ajira@immigration.go.tz

Limetolewa na;

KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI
MAKAO MAKUU DODOMA

13 Aprili, 2026